


Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 2 , 2015

Bei Sh. 800



NDANI

M dahalo kuhusu
utambulisho wetu
Wahitimu udaktari
Nafasi za masomo
Majilio na Krismas
ni nini?
Fahamu sababu za
kukumbuka
watakatifu KKKT

EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA

RE-ADVERTISEMENT

The ELCT - Head Office in Arusha invites applications from experienced, competent, proactive team players, and self driven persons to fill the position of:

AUDITOR GENERAL

The AUDITOR GENERAL heads the Audit Division and is responsible to ELCT Executive Council through the ELCT Audit Board.

TERMS OF SERVICE

He/She will be appointed on a five (5) years contract basis renewable.

SPECIFIC DUTIES WILL INCLUDE

1. Prepares audit plans
2. Liaises and solicits clients
3. Signs audit reports
4. Responsible for staff performance
5. Participates in significant audit decisions
6. Conduct general review of the audit file
7. Quality assurance of the final report
8. Communicate to clients regarding audit issues
9. Prepares department's annual reports
10. Facilitates audit Board meetings
11. General administration of the Department.

QUALIFICATION AND EXPERIENCE

1. CPA (T), ACCA or equivalent, should be registered by NBAA in the category of Associate or Fellow in Public practice.
2. Master of Business Administration (MBA) will be added advantage.
3. At least up to 5 years experience in a senior audit position and able to produce quality work within the set deadlines.
4. Have good analytical and organizational skills.
5. Good communication and interpersonal skills.
6. Computer literate.
7. At least 40 years of age

SALARY AND BENEFITS:

As per ELCT Common Works salary scales.

MODE OF APPLICATION

- Applications should be attached with copies of relevant certificates and CVs.
- Applicants should give the names of three reputable referees with their contact information including; address, telephone /email/Fax numbers.
- Applicants are required to obtain an endorsement from their respective Diocesan General Secretaries.
- All applications should be addressed to the Secretary General of the Evangelical Lutheran Church in Tanzania, P.O. Box 3033, Arusha Tanzania and should reach him not later than 31 December, 2015.



Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi.

Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

Mhariri
Uhuru na Amani
S.L.P. 3033
ARUSHA

Barua pepe: elobulu@elct.or.tz
sms kwa Mhariri: 0754-482-285
WhatsApp: +255-754-482-285
Fungua Tovuti ya KKKT:
<http://www.elct.org/>

MHARIRI **Elizabeth Lobulu**

Limepigwa Chapa na:
Moshi Lutheran Printing Press
S.I.P 301 Moshi
lutheranpress@yahoo.com

Newspaper Design & Typesetting:
Elizabeth Lobulu

Wachangiaji wa Makala:

Mch. Dkt. Rose Materu
Mch. Thomas Maumbuka
Mch. Prof. Gwakisa Mwakagali
Askofu Dkt. Owdenburg Mdegella
Mch. Dkt. Faustin Leonard Mahali
Mallumbo William Mallumbo
Mch. Dkt. Anneth Munga
Faustine Nillan Losai
Felix Mwetha
**PICHA NA: Deo MOSHA &
PHILEMON FIHAVANGO/ SYI**

PICHA YA JALADA:

Askofu Dkt. Fredrick Onael Shoo,
aliyechaguliwa na Mkutano Mkuu wa 19
wa KKKT Agosti 2015 kuwa Mkuu wa
KKKT. **PICHA NA DEO MOSHA/ SYI.**

MAONI YA MHARIRI

Makanisa yetu hapa Tanzania na kwingineko duniani yanapita katika kipindi ambacho roho ya kutolipenda Kanisa inaongezeka mionganoni mwa watu wa karne hii.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Askofu Dkt. Alex Malasusa ambaye pia ni Makamu wa Rais Kanda ya Afrika katika Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani alipofungua Mkutano Mkuu wa 19 wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Alisema ni kipindi ambacho mafundisho ya Yesu Kisto ya kumpenda jirani na kumpenda adui yanapata changamoto.

Alieleza kuwa tunapita kipindi ambacho ile misingi yetu ya imani inatiliwa mashaka na kutafsiriwa vinginevyo ili kukidhi matakwa yetu kama wanadamu.

Alisema nyakati hizi ambapo mifumo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni inachochea roho ya ubinafsi, Kanisa linahitaji umoja ili kufanya utetezi dhidi ya mifumo kandamizi.

Yesu alipowaombea wanafunzi wake umoja (Yn 17: 21) alikuwa pia anahimiza umoja mionganoni mwetu na kwamba alikuwa anahimiza umoja ili uwe utambulisho wetu katika misheni ya Mungu kwa ulimwengu wote. Kwa kifupi ujumbe ni kwamba Kanisa linapaswa kuwa na umoja wa dhati.

Alisema iko misemo mingi inayohimiza umoja kama vile: ‘Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu’. “Usemi huu maana yake kwetu sisi Kanisa na hasa tunapozingatia utume wetu kwenda kwa kila kiumbe kuhubiri Injili, endapo tutapanga kwa pamoja na tukifanya uinjilisti kwa pamoja, tukiomba kwa umoja Kanisa la Bwana litaongezeka, alifafanua. Alitoa mfano wa Wilaya ya Itilima, Mkoani Simiyu eneo la KKKT Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria, eneo ambalo wako watu wengi hawajasikia Injili ya Yesu Kristo.

Alisema baada ya kutembelea eneo hilo la misioni alijionea mwenyewe kwamba watu wengi hawana huduma muhimu za kijamii kama shule, maji safi na salama, zahanati wala kanisa. Idadi kubwa ya wakazi wake hawana dini na hawamwamini Mungu bali wanaamini zaidi uchawi na ushirikina kiasi ambacho waganga wa kienyeji ni wengi sana kwa ajili ya tiba za asili au ramli.

Hivyo alisema: “Ndugu zangu (wajumbe na washarika kwa jumla) tunahitaji kushirikiana katika kazi hiyo ya uinjilisti katika maeneo mbalimbali katika Kanisa letu. Ni dhahiri tukifanya kwa pamoja tutafanikiwa”.

Kanisa lampongeza Rais Awamu ya Tano



Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, akinua mkuki na ngao, vitu alivyokabidhiwa baada ya kuapishwa kuwa Rais 5 Novemba 2015. Nyuma yake ni Rais wa Awamu ya Nne, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais, Dkt. Gharib Bilal.

Ni Askofu Keshomshahara Kaskazini Magharibi

Makamu wa Rais wa Serikali ya Awamu ya Nne, Mheshimiwa

Dkt. Gharib Bilal akimpongeza Mkuu mpya wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi, Askofu Dkt. Abednego Keshomshahara (aliye na fimbo ya uaskofu), baada ya Ibada ya kumweka wakfu huku Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa akitazama.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) Askofu Dkt. Alex Malasusa, ambaye pia ni Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), amempungeza Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyeapishwa 5 Novemba 2015 baada ya kushinda kura zilizopigwa 25 Oktoba.

Mkuu wa KKKT alikuwa mionganoni mwa viongozi watatu wa dini waliopewa nafasi ya

Watumishi watatu waagwa

Watumishi watatu wa Ofisi Kuu ya KKKT waliagwa hivi karibuni baada ya kumaliza mikataba ya kutumikia Kanisa katika nafasi mbalimbali.

Watumishi hao ambaowanaonekana wakikata keki kutoka kushoto ni Bw. Richard Mwakatundu aliyekuwa Mratibu wa Huduma ya Afya ya Msingi KKKT kwa miaka 12. Hata hivyo Bw. Mwakatundu anayetoka Dayosisi ya Kaskazini Magharibi ana jumla ya miaka 35 ya utumishi katika Kanisa.

Anayefuata ni Bw. Abel Mrema aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala KKKT kwa miaka sita na kulia ni Bw. Gideon Mbalakai aliyekuwa Mhasibu katika Kurugenzi ya Afya aliyetumikia KKKT miaka 18.

kufanya maombi kabla Rais Magufuli hajaapishwa.

Alimshukuru Mungu kwa kuivusha nchi salama katika uchaguzi na kutoa wito kila mtu ajitahidi ili nchi iendelee kuwa ya amani.

Aliwaombea viongozi wa Serikali hekima kutoka kwa Mungu katika kunena na kutenda. Alitaka wajitahidi kuwaunganisha watu wote ili upendo, amani, umoja wa kitaifa na uzalendo uwepo nchini.



Mchungaji Dkt. Abednego M. Keshomshahara aliwekwa wakfu 18 Oktoba 2015 katika Kanisa Kuu la Kilutheri Bukoba mjini kuwa Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi. Aliwekwa wakfu na Askofu Elisa Buberwa aliye maliza kipindi cha kuingoza dayosisi hiyo.

Ibada hiyo ya wakfu ilihudhuriwa na Makamu wa Rais Dkt. Gharib Bilal (aliywakilisha Serikali); Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa (aliyemwingiza kazini Askofu Abednego); viongozi wengine wa KKKT wakiwemo Maaskofu, Wachungaji, Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, Washarika na wageni toka ndani na nje ya nchi wakiwemo wajumbe wa Mkutano wa 'LMC Roundtable' waliokuwa wamefika kwa ajili ya mkutano uliofanyika Bukoba.

KKKT na Sikukuu ya Watakatifu

Na Mch. Dkt. Faustin Leonard Mahali



Mch. Dkt. Faustin Leonard
Mahali, Naibu Makamu
Mkuu Taaluma Chuo Kikuu
cha Tumaini Makumira.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) husherehekeea Sikukuu ya Watakatifu kila mwaka. Katika kalenda yake, sikukuu hii imewekwa wiki nne kabla ya Majilio.

Hata katika utaratibu wa Ibada ya Ushirika Mtakatifu, Mchungaji huwaongoza Washarika kuungana na "malaika wakuu na mababa, manabii, mitume na mashahidi na jeshi la mbinguni pia" ili

wamtukuze Mungu ambaye ndiye Mtakatifu, (TMW uk. 365). Katika kuimba Zaburi washarika kama watakatifu wanahimizwa nafsi zao zijisifu na kumcha Bwana (TMW uk. 396).

Ahadia ya Mungu kwa wale wote wanaoishi katika ushindi wa imani ni kuvikwa taji la uzima, (TMW uk. 452). Hivyo sifa na tukuzo ndani ya KKKT hufanywa na washarika wote walio hai na wale waliolala katika Bwana.

Kutokana na msingi huu KKKT imeweka pia utaratibu wa kuwakumbuka ndugu, jamaa, na marafiki waliotutangulia "katika haki" kama inavyojulikana siku hizi.

Mojawapo ya maombezi ya sehemu ya kwanza inasema: "Wewe Bwana na Mwokozi, Yesu Kristo, uliye mwaminifu, umwongoze (ndugu yetu/ rafiki yetu)

kwenye nuru ya Mungu na kumfikisha katika kundi la watakatifu," (TMW uk. 607). Jambo hili pengine ndilo lenye utata mkubwa kwa sasa na hivyo kuhitaji maelezo ya kina ili ibada hii iwe ya baraka kwetu sote.

Neno "takatifu," kwa Kiyunani "hagios" na Kilatini "sanctus" lilitumika katika hali ya kawaida kumaanisha mtu mtakatifu au kitu kitakatifu. Katika dunia ya 'kipagani,' mfalme, miungu, ndugu waliokufa, nk. walipewa sifa ya utakatifu.

Katika dini ya Kikristo, Maaskofu, Wachungaji Wazee wa Kanisa, bikira Mariamu, wafia dini, watawala wacha Mungu waliolala, wote waliitwa watakatifu kwa sababu ya matendo yao yaliyotukuka.

Katika habari hii ni vizuri tukaainisha watakatifu katika makundi matatu: Kwanza, watu walioishi maisha ya kishujua na uadilifu mkubwa. Pili, watu tunaofikiri (kwa kipimo chetu) kwa imani yao

wanakwenda mbinguni - na hawa ndio tunaowakumbuka katika taratibu zetu za ibada kama ilivyoonyeshwa katika utangulizi.

Tatu, watu waliopita mchakato na kutambuliwa kuwa wenye heri na baadaye watakatifu. Watakatifu wa kundi la tatu huabudiwa na kufikiriwa kuwa na nguvu ya kuleta mabadiliko ya kimwili na kiroho kwa wale wanaoabudu.

Martin Luther ndiye aliyeweka msingi wa kutokuwa na mkazo unaoeleweka kuhusu ibada za watakatifu. Alisema: 'kuenzi watakatifu fulani ni ibada za sanamu; watakatifu hawawezi kuwa wawakilishi wa mambo yetu kwa Mungu isipokuwa Kristo tu na kwamba watakatifu si kana kwamba wana neema zaidi ya Mkristo mwingine awaye yote hata kama matendo yao yatakuwa mema kiasi.'

Mawazo haya hayafuti kuwa na Sikukuu ya Watakatifu. Badala yake yanahimiza kufanya ibada ya kumsifu na kumcha Mungu wakristo wote au kwa maana nyingine watakatifu wote. Hivyo si dhambi kuungana na ndugu, jamaa na marafiki kumsifu na kumtakuza Mungu.

Lakini kufikiri kwamba kwa njia ya ndugu, rafiki na jamaa zako waliokufa unawezesa ukapata bahati na kupokea baraka hiyo ndio dhambi. Ikumbukwe kuwa baraka ni ya Mungu na tunapata kwa neema tu. Lakini hii haimaanishi tuisiwakumbuke jamaa, marafiki na ndugu zetu. Tunapaswa kuungana na kuwakumbuka watakatifu walio hai na wafu ili kuendelea kumsifu na kumtakuza Mungu katika maisha yetu. Huu ndio msingi wa Kilutheri wa Sikukuu ya Watakatifu. Kwa maoni wasiliana na Mch. Dkt. Faustin Leonard Mahali, Mhutubu Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira: +255 754 040 589

Wanafunzi wa uganga wafanya ziara KKKT



Hivi karibuni wahitimu na wanafunzi wa udaktari toka Dayosisi za KKKT walitembelea Ofisi Kuu ya KKKT. Kaimu Mkurugenzi wa Afya KKKT, Dkt. Zebadiah Mmbando (wa kwanza kulia), alisema madhumuni ni kuwakutanisha uongozi na wanafunzi wahitimu ambao wamepata uhisani kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Amerika (ELCA). Gharama ya mwanafunzi mmoja ni sh. milioni 16 kwa mwaka na mtu mmoja anasoma miaka sita - mitano chuoni na mwaka mmoja wa mazoezi kwa vitendo.

Bw. Mallumbo W. Mallumbo, Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo KKKT (wa tatu kutoka kulia), alitoa shukran kwa Kanisa la Amerika kwa msaada wa kusomesha wanafunzi hao. Aliwashauri wanafunzi wafanye bidii na kuwaasa waliohitimu watimizie viapo vyao kwa kufanya kazi kwa bidii watoapo huduma hospitali za Kanisa watakazopangiwa kwa kuzingatia kanuni na mikataba iliyopo. Wakati wa hafla fupi ofisini hapo, Bw. Mallumbo, alimkabidhi Dkt. Christopher Arrip Kipuvyo aliyekuwa amehitimu masomo ya Udaktari kwa Katibu Mkuu Msaidizi wa Dayosisi ya Kaskazini Kat, Mch. Jasson Kahemba na Katibu wa Afya Dayosisi hiyo, Dkt. Simon Megiroo.

Pichani kutoka kushoto: Bibi Barbara Hinderlie Mwakilishi ELCA nchini akifuaatiwa na Loveness John (Dayosisi ya Kaskazini) ambayo yuko mwaka wa Nne Hubert Kairuki Memorial University (HKMU), Dar es Salaam; Dkt. Kipuyo (Dayosisi ya Kaskazini Kat) aliyehitimu Shahada ya Udaktari Chuo Kikuu cha IMTU, Dar es Salaam. IMTU ni 'International Medical and Technological University'. Anayefuata ni Victoria Adonicam (Dayosisi ya Kaskazini) mwaka wa Nne Chuo cha HKMU; Lightness Gudu (Dayosisi ya Kat) mwaka wa Kwanza Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na Moses Isaya (Dayosisi ya Kat) mwaka wa Kwanza Kampala International University, Dar es Salaam. Wanafunzi wengine watatu hawakuweza kufika.

Fahamu maana ya majilio

Na Mch. Thomas Maumbuka

‘Majilio; ni neno la Kilatini lenye maana ya “kuja” au “kufika” (adventus) - hasa kuja kwa kitu ambacho kina umuhimu mkubwa na wa kipekee.

Kipindi cha majilio huanza majuma manne kabla ya Sikukuu ya Krismas, Disemba 25 au siku ya kukumbuka kuzaliwa kwa Yesu Kristo ambayo huwa ni Jumapili iliyo karibu na Novemba 30 na kuishia Disemba 24.

Kwa Kanisa letu la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Majilio ndio mwanzo wa Mwaka Mpya wa Kanisa.

Mkazo mkubwa katika kipindi hiki ni kusherehekeea kuzaliwa kwa Yesu Kristo siku ya Krismasi na matazamio ya kurudi kwa Yesu Kristo Mfalme mara ya pili.

Majilio ni kipindi cha maandalizi ya kiroho ambapo wakristo wanajiandaa kukumbuka kuzaliwa kwa Yesu Kristo au kuja kwa Mfalme siku ya Krismasi.

Hivyo wanapaswa

kuelekeza miyo na mawazo yao kumngaja Yesu kuja mara ya pili kulichukua Kanisa. Kwa maana hii, majilio ni kipindi cha mashangilio na matumaini ya kiimani.

KUSUDI LA KANISA KUWA NA MAJILIO

Kusudi la Kanisa kuadhimisha au kuwa na kipindi cha majilio cha kumngaja Bwana si tu kwa kumshukukuru Mungu kwa ukombozi, kwa kuzaliwa kwa Yesu Kristo au kuja kwa Yesu Kristo duniani kwa mara ya kwanza kama mwanadamu, bali pia kwa uwepo wake katikati yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu, na matarajio makubwa au matumaini makubwa ya kuja kwa Yesu mara ya mwisho kulinyakua Kanisa. **“Tazama, mfalme wako anakuja kwako; Ni mwenye haki, naye ana wokovu...”** (Zak. 9:9b).

Nia ya kipindi hicho ni kuwakumbusha Wakristo kupata nafasi ya kutafakari Neno la Mungu kwa pamoja



Mch. Thomas Maumbuka

na pengine kwa kupitia vifungu maalumu katika Biblia. Ni kipindi cha kuweka mkazo katika sala na maombi pamoja na kutubu kukifatiwa na matarajio ya matumaini ya furaha ya ukombozi.

Sababu nyingine ni ili kuwavuta Wakristo karibu zaidi na Mungu wao kwa njia ya mafundisho, nyimbo za mashangilio na Liturgia hasa katika kipindi hicho cha mapumiziko ya kazi za kila siku ambapo kwa wengi ni kipindi cha likizo; hivyo kusauhau taabu, hofu na changamoto za maisha ya kila siku na kuelekeza mawazo yao kwa Yesu Kristo mkombozi wao.

Katika Kitabu cha Tumwabudu Mungu Wetu Wimbo Namba 10, ubeti wa 1 una maneno haya:

*“Bwana anakuja twendeni kumlaki
Bwana Mungu wa majeshi,
Iwasheni miyo tukampokee
Huyo mwenye utukufu.
Karibu Bwana, njoo.
Karibu Bwana, njoo.
Shinda pamoja nasi.*

Lakini si hivyo tu, bali majilio ni kipindi cha kila Mkristo kwa maisha yake binafsi kujitoa na kupata faragha na Mungu wake kwa kusoma Neno la Mungu kila siku, kutoa muda wa ziada kwa maombi ya binafsi, familia, Kanisa na taifa; kuwatemelea majirani na kuwatia moyo ili kumngaja Yesu Kristo hasa kwa walio kata tamaa; kuwatemelea wagonjwa na wasiojiweza na kushiriki pamoja nao katika maombi na hati ikiwezekana kuwasaidia wahitaji.

Majilio si kipindi tu cha maandalizi ya kihistoria

ya kusherehekeea kuzaliwa kwa Yesu Kristo siku ya Krismasi, bali ni mwanzo wa kuadhimisha muujiza wa Mungu kufanyika mwanadamu (incarnation) kwa njia ya ajabu mno na kisha kukaa pamoja nasi.

Kuja kwa Yesu Kristo kultibiriwa tangu zamani na manabii wa Agano la Kale:

“Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa tumepewa mtoto mwanamume na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake, naye ataitwa jina lake mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele mfalme wa amani” (Isa 9:6). Pia “**Furahi sana Ee binti sayuni, piga kelele Ee binti Yerusalemu tazama mfalme wako anakuja kwako**” Zek 9:9.

Kanisa linakumbushwa kwamba linaishi katikati ya vipindi viwili vya kihistoria: kuja kwa Yesu Kristo kwa njia ya mwili (flesh) duniani na kuja kwa utukufu siku ya mwisho kulinyakua kanisa. Hivyo kanisa linapaswa kuwa imara katika imani hasa tunapongojea kwa furaha na matumaini kuja kwa mwokozi wetu Yesu Kristo. Utawala wa Mungu uko katikati yetu lakini bado haujafunuliwa katika ukamilifu wake.

Wakristo tunaadhimisha kile ambacho tayari tunacho lakini wakati huo huo tukitaraji kile kitachofunuliwa baadaye kwa ukamilifu kama anavyosema Mtume Paulo kwamba sasa tunaona kwa kioo lakini **tutaona uso kwa uso**.

Kipindi cha majilio sisi tulio wakristo tutegemee kufanywa au kuumbwa upya miyo yetu na kuwa tayari kumpokea Yesu Kristo kwa upya miyoni mwetu, kutengeneza maisha yetu, kugeuka na kuacha njia mbaya na kuweka ukristo wetu katika vitendo na si katika maneno tu.


Nyakati hizi ujumbe muhimu wa majilio ni ‘tubuni kwa maana ufalme wa Mungu umekaribia’.

Mch. Maumbuka ni Mratibu Dawati la Nishati Jadidifu katika Kitengo cha Uhai na Mazingira KKKT. Anapatikana kwa sms: +277 768 424 408

Nafasi za masomo katika mitandao

Vyuo hivi vinatangaza nafasi za masomo lakini **HAINA MAANA KWAMBA KANISA LINAHUSIKA**. Hivyo kwa aliyetayari kujaribu afungue viungo ([link](#)) vya tovuti na kuwasiliana na vyuo husika na kuzingatia masharti na vigezo vyao:

1. 2016 Norway Quota Scholarship Scheme for students of Developing Countries --- <http://www.afterschoolafrica.com/682/scholarship-in-norway-for-bachelors>
2. USA Government Scholarship--- http://www.aminef.or.id/index.php/pia_fungua <http://www.iief.or.id>
3. Netherland Government Scholarship--- <http://www.nesoindonesia.or.id/beasiswa>
4. Belgium Government Scholarship--- <http://www.vliruos.be/4273.aspx>
5. Utrecht University Netherland --- <http://www.uu.nl/.../grantsandscholarships/Pages/utrechtexcel>
6. University of Twente Netherland--- <http://www.utwente.nl/international.../scholarshipsandgrants/.../>
7. Sweden Government Scholarship --- <http://www.studyinsweden.se/Scholarships/>
8. Panasonic Scholarship Japan --- <http://panasonic.net/citizensh.../scholarships/.../requirements/>
9. Ancora Foundation Scholarship--- <http://ancorafoundation.com>
10. Asian Public Intellectuals Fellowship Japan--- <http://www.apifellowships.org/body/>
11. School of Government and Public Policy Indonesia--- <http://sgpp.ac.id/pages/financial-conditions>
12. Macquarie University Australia (http://www.mq.edu.au/.../macquarie_university_international_.../



Askofu Dkt. Frederick Shoo,
Mkuu mteule wa KKKT ataingizwa
kazini 31 Januari 2016 mijini Moshi
katika Kanisa Kuu la KKKT Dayosisi
ya Kaskazini. Pichani juu Askofu
Dkt. Shoo alipokuwa akiwashukuru
wajumbe baada ya kuchaguliwa.

TOLEO MAALUMU

Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT



Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Gehaz Malasusa (katikati) aliongoza Ibada ya kufungua
Mkutano Mkuu akisaidiwa na Askofu Dkt. Paulo Akyoo na Mch. Dkt. Msafiri Mbili.



Askofu Dkt. Alex Malasusa,
Mkuu wa KKKT anayemaliza muda
wake baada ya kutumika kwa
vipindi viwili nya miaka minne
minne. Katiba ya KKKT inaruhusu
kuchaguliwa kwa vipindi viwili tu.



Maandamano kabla lbada
ya Ufunguzi kuanza.



Kwaya ya Matarumbeta kutoka Dayosisi ya Meru.



Kwaya kutoka Dayosisi ya Mashariki na Pwani.



Viongozi wa Kanisa wakati wa Ibada ya Ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa 19.



Baadhi ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa KKKT 2015.

Akishiriki Mdashalo kuhusu "Umoja na Utambulisho wa KKKT" Profesa Dkt. Joseph Parsalaw, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, alitaka viongozi



Askofu Dkt. Shoo akiongea jambo na Mchg. Profesa Parsalaw na Mchg. Dkt. F. Mahali mara baada ya kuchaguliwa kuwa Mkuu wa KKKT Agosti 2015.

wa Kanisa waseme yale yaliyo kweli kuhusu wokovu na siyo kuwaacha watu wakipotoshwa. Wapo washarika wanaokwenda kuchukua mafuta ya mizeituni na chumvi toka Israel na



Katibu Mkuu wa KKKT Bw. Brighton Killewa (katikati) akishauriana jambo na Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala, Bw. Loata Mungaya (kulia) kabla ya Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT kuanza. Wengine ni Patricia Mwaikenda na Mchg. Lazaro Rohho anaeonekana nyuma yao.



Baadhi ya Maaskofu waliohudhuria Mkutano Mkuu wa KKKT 2015.

baadhi wanakwenda Nigeria kuchukua maji ya TB Joshua kwa imani kwamba watatatuwa matatizo yao kwa kutumia vitu hivyo.

Profesa aliwaambia

wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT kwamba kuamini vitu hivyo ni sawa na ushirikina.

Alisema kwamba safari za 'hija' hazimwongezei mtu chochote katika wokovu bali huo ni utalii.

Kuhusu mafundisho ya sadaka ya ukombozi wa mzaliwa wa kwanza au sadaka ya utajirisho alisema hayo ni mambo yaliyokatazwa na wana matengenezo kwa kuwa hakuna tofauti na sadaka iliyotolewa ili mtu apate cheti cha msamaha wa dhambi na alisitisiza kwamba **wokovu hauuzwi**.

Wajumbe wajadili umoja na utambulisho wa Kanisa

Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa alipofungua Mkutano wa 19 wa KKKT 11 Agosti 2015 alisema kukosekana kwa toba katika Jamii yetu kumesababisha amani kutoweka tangu ngazi ya familia hadi taifa. (Soma zaidi uk. 3).

KUKOSEKANA KWA TOBA

Akjadili suala hilo Yvonne Mmbando njumbe kutoka Dayosisi ya Mashariki na Pwani alisema mahali ambapo Mungu hayupo maana yake hapo mahali shetani yupo; na kazi yake ni kuharibu, kuua na kuchincha.

Neno la Mungu linasema usiposamehe na wewe hutasmehewa. Kwa hiyo toba inakufanya uwe karibu na Mungu na hapo tabia ya Mungu ya huruma na unyenyeketu itakuwa ndani yetu na toba itatuwezesha kudumisha amani.

TUFUATE LITURJIA YETU

Kuhusu wanaoingiza mambokinyume na liturgia na Ibada za KKKT, Askofu Ambele Mwaipopo wa Dayosisi ya Ziwa Tanganyika, alisema KKKT ina liturjia inayombwa katika melodias inayolitambulisha. Jambo hilo linaonekana katika Ibada



DONDOD MUHIMU

Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT uliofanyika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira 12 - 14 Agosti 2015 ulikuwa na Neno Kuu "Jitahidi kuuhifadhi Umoja wa roho katika kifungo cha Amani" (Efeso 4: 3) ambalo lilitumita kwa ajili ya Somo la Biblia.

Askofu Dkt. Frederick Shoo ambaye ni Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini alichaguliwa kuwa Mkuu wa Kanisa. Pia Bibi Alice Mtui kutoka Dayosisi ya Konde alichaguliwa kuwa Mwandishi. Wengine waliochaguliwa ni Wajumbe wa Halmashauri, Kamati na Bodi za Kanisa.

Eneo la Mwanga katika Dayosisi ya Pare limekubaliwa kuijandaa kuwa Dayosisi.

Mada tatu zilizoongozwa na Kauli mbii: *Umoja na Utambulisho Wetu* zilitolewa. Mada kuhusu *Umoja na Utambulisho Wetu katika Kuwajibika* alipewa Mch. Dkt. Rose Materu; *Umoja na Utambulisho Wetu katika Kuabudu* iliongozwa na Askofu Dkt. Owdenburg Mdegella na Mch. Dkt. Anneth Munga aliongoza mada kuhusu *Umoja na Utambulisho Wetu katika Huduma ya Neno na Sakramenti*.

Upupisho wa mada unapatikana katika ukurasa wa 10 hadi 12 wa toleo hili la Gazeti la *Uhuru na Amani*. *Pia fungua tovuti ya KKKT: www.elct.org kwa picha na maelezo zaidi*.



Bibi Alice Mtui kutoka Dayosisi ya Konde alichaguliwa na Mkutano Mkuu wa 19 kuwa Mwandishi wa KKKT kwa miaka minne kuchukua nafasi ya Bibi Happiness Gefi kutoka Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria ambaye alitumikia nafasi hiyo kwa miaka 4.

mbalimbali ikiwemo Ibada ya Siku ya Bwana, nk.

Katika Ibada hizo vipengele kadhaa huizingatiwa kama kuhubiri, kufundisha, kukiri, kutubu, kuomba, kusifu, nk. Na mambo hayo yamewekwa vizuri katika maandiko ya KKKT kama Kitabu cha Tumwabudu Mungu Wetu (TMW). Nahimiza tutumie nyenzo hizo na kufuata taratibu zinazotutambulisha kuliko kuiga vitu ambavyo wakati mwingine haviongezi kitu.

MAPAMBIO KATIKA IBADA

Kuhusu baadhi ya watu kupenda kuimba 'mapambio' badala ya nyimbo za TMW, Mch. Gideon Paulo Kivuyo, Msaidizi wa Askofu Dayosisi ya Kaskazini Kati, alisema ni kwa kuwa wakati mwingine haziimbi inavyopasa. Na wakati mwingine maandalizi ya nyimbo na Ibada kwa ujumla ni duni. Ndio sababu baadhi ya watu huvutwa na mtindo wa makanisa ya Kipentekoste kwa kuimba mapambio badala ya nyimbo za TMW. Lakini muundo wa Ibada za KKKT unahitaji maandalizi na si Ibada rahisi kama za kuimba tu mapambio.

Ebenezer Shao, Mwenyekiti wa Vijana KKKT, alisema mafunzo ya 'Injili ya Utajirisho' siyo


sahihi kwa kuwa haitulazimu kumhonga Mungu kwa sadaka zetu ili atubariki. Mungu hutubariki na kututajirisha pale tunapoishi maisha ya utaua.

Sista Kokushaba Kiiza toka Dayosisi ya Karagwe alisema Kanisa lifanye juhudzi zaidi washarika wapate mafunzo zaidi ili wasitamani mifumo ya Ibada zilizo nje ya Ulutheri. Mafunzo hayo yaanzie katika Shule za Jumapili, Kipaimara na vipindi vya Elimu ya Kikristo shulenii ili vijana waive vya kutosha kuhusu Ulutheri wetu. Pia wanafunzi wa Theolojia na Wachungaji waive vizuri kuhusu liturgia na taratibu za Ibada kwa jumla.

KUTUNZA KAZI ZA UMOJA

Profesa Esther Mwaikambo Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maoni alisema ili kuhakikisha michango kwa ajili ya Kazi za Umoja inafika kwa wakati; pawepo ufuatilaji wa karibu wa Ofisi Kuu kukumbushia mara kwa mara kwa barua.



Askofu Lucas Mbedule wa Dayosisi ya Kusini Mashariki alitoa wito viongozi na washarika kuzingatia na kufuata taratibu tulizojiwekea ili kulinde umoja.



Mch. Dkt. Fidon Mwombeki, Katibu Mkuu wa United Evangelical Mission (UEM), iliopo Ujerumanu aliusalimu Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT.



Mch. Rachel Axwesso (juu), Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii na Kazi za Wanawake na Watoto KKKT, alitoa taarifa kuhusu Kongamano la Jubili ya Miaka 25 tangu KKKT ikubali kubariki wanawake kuwa Wachungaji. Pamoja na mambo mengine Kongamano illimpongeza Mch. Alice Kabugumila (mwenye vazi la Ibada na stola nyekundu) aliyekuwa mwanamke wa kwanza kusomea theolojia Afrika kwa kuvumilia miaka 35 baada ya kuhitimu mafunzo ya theolojia kabla yake kubarikiwa kuwa Mchungaji katika Dayosisi yake ya Kaskazini Magharibi.



Mkuu Mstaafu wa KKKT Askofu Dkt. Samson Mushemba aliasalimu Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT.

UMOJA NA UTAMBULISHO WETU KATIKA **Kuwajibika**



**Mchg. Dkt. Rose Materu
Mhutubu Chuo Kikuu Kishiriki cha
Kumbukumbu ya Stefano Moshi.**

Na Mch Dkt. Rose Materu
Utanqulizi

Umoja wa Kanisa umeanzishwa na roho ya umoja walijokuwa nayo waanzilishi wa Kanisa 1963 walipounganisha makanisa saba na kuunda Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanganyika (KKKT). Wanakanisa wa leo tuhimize roho ya umoja kwa ufanisi wa shughuli za pamoa kama kazi za misioni ndani na nje ya nchi, huduma za elimu, afya, diakonia na miradi ya maendeleo.

KKKT ni mwanachama wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania; Baraza la Makanisa ya Afrika; Jumuiya ya Makanisa ya Kilutheri Afrika Mashariki na Kati (LUCCEA); Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani na Baraza la Makanisa Duniani. Kuwa mwanachama maana yake ni kushiriki kutoa michango ya kusaidia kazi za pamoa na kushiriki kikamilifu katika masuala yote yanayohusu jumuiya hizo; jambo ambalo KKKT imekuwa mstari wa mbele. Sio makanisa yote duniani ni wanachama wa jumuiya hizo. Hiryo katika hili pia tunawiwa kuwashukuru waasisi wetu wa KKKT kwa maono ya kuliunganisha kanisa letu na jumuiya hizo tanqu mwanzo.

Umoja na utambulisho wetu Wana-KKKT unaonekana katika imani, theologia na mafundisho ya Kilutheri. Kanisa lina maandiko yanayotumika katika huduma. Maandiko ni muhimu sana kwa mafundisho ya watoto ambaeo tunataka walifahamu Neno la Mungu kwa usahihi ili wawewe kusimama imara katika imani na ufuasi wao na kuwa waumini

wazuri wa kanisa letu hasa katika kipindi hiki ambacho kuna mafundisho ya kila aina na kila mahali. Machapisho ya Kanisa yana nembo ya KKKT ambayo inatutambulisha vizuri.

Kitabu cha Mwanzo 2: 15 kinalezea
Mungu alipomuuumba mwanadamu wa
kwanza alimweka katika bustani ya Edeni na
kumuagiza alime na kuitunza; hivyo ni muhimu
kila mwanadamu afanye kazi ili kupata riziki
kwa ajili ya maisha yake ya siku kwa siku.
Kwa hiyo, tunapofanya kazi tunatimiza agizo
la Mungu. Wakristo wanawea kuchangia
Asilimia mbili (2%) na Sadaka ya Siku ya
KKKT kila mwaka kwa sababu wanafanya
shughuli mbalimbali zinazowapatia kipato.

Katika Injili ya Mathayo 28:18-19 tunaona Wakristo walivyoshiriki kwa hali na mali katika kueneza Injili ya Yesu Kristo. Sadaka za Wakristo, ziara za Uinjilisti, rasilimali watu, Kwaya mbalimbali na vipawa mbalimbali Mungu aliviyoviweka ndani ya watu wake vimesaidia kuwafikishia watu **Habari Njema** za Yesu Kristo; hivyo Kanisa la Mungu limeongezeka siku kwa siku.

Umoja wetu katika uwajibikaji unajidihirisha katika ile picha ya mwili wa Kristo kwamba tunategemeana. Kila kiungo katika mwili kina wajibu wake wa kufanya na vinategemeana (IKor. 12: 15). Uwajibikaji wetu uitaonekana kwa jinsi ambavyo kila dayosisi inatekeleza mapatano na maamuzi yanayoamuliwa katika vikao mbalimbali na hasa Mikutano Mikuu ya KKKT.

Sadaka na michango ya pamoja ni kielelezo cha umoja. Mchango wa asilimia mbili (2%) ya KKKT na sadaka ya Siku ya KKKT inayotolewa mwezi Juni kila mwaka ni fedha zinazotunza Kazi za Umoja katika Kanisa letu. Sadaka

hizi hutolewa na Wakristo wa marika yote – watoto, vijana na watu wazima. Uaminifu wa kila dayosisi kuwasilisha fedha hizi katika hazina kuu ya Kanisa kwa wakati unaotakiwa ni alama ya kuwajibika na kudumisha umoja wetu. Kwa hiyo, kuchelewesha au kutokuhawasilisha mafungu haya hukwamisha shughuli hizi.

KKKT iliamua kuwabariki wanawake kuwa wachungaji 1990. Dayosisi nyangi zimetekeleza uamuzi huu. Umoja umeonekana katika matamko ya pamoja kama **Tamko la Bagamoyo na Tamko la Dodoma**: Ujasiri wa viongozi wetu wa KKKT kujadili kwa pamoja mambo magumu wanayoyaona kuwa yataliweka Kanisa au taifa letu mahali pabaya ni jambo zuri la kuigwa na wengine maana kwa kufanya hiyo kanisa linatimiza wajibu wake wa kuwa **sauti ya kinabii**. Misimamo tofauti mionganoni mwetu katika masuala yanayojitokeza katika nchi yetu italeta shida, maana maadui watatumia nafasi hiyo kutuqawa.

Kanisa lina vituo vingi vya pamoja ambavyo vinatoa huduma kwa jamii yetu bila ubaguzi wa dini wala kabilা. Kuna **Seminari Ndogo ya Kilutheri Morogoro, Shule za Msingi na Sekondari Mwanga na Njombe** (watoto viziwi). Tabia na mienendo yenyе ushuhuda mzuri kwa watumishi na wanafunzi itiliwe mkazo kwa shule zetu zote.

Kazi ya misioni ya KKKT: Hakuna kanisa kama hakuna misioni. Kanisa la Mungu linakua kwa kasi kwa sababu ya kazi ya misioni na unjilisti inayofanyika ndani na nje ya nchi yetu. Umoja wetu katika kupeleka watumishi katika maeneo haya ya misioni imeongeza idadi ya Walutheri katika nchi yetu na nchi jirani.

Ushirikiano wa watumishi wachache waliopelekwa katika maeneo hayo kutoka katika dayosisi zetu na Wakristo wachache waliooko katika maeneo husika umewaleta wengi kwa Kristo. Wakristo wa kawaida wamejitoa kwa hali na mali kusaidia kazi ya Injili katika maeneo haya. Nyumba za Ibada zimejengwa, vyombo vyua usafiri kwa watumishi vimenunuliwa, vituo vingi vya huduma pia vimefunguliwa ili kumhudumia mwanadamu kwa ukamilifu.

Dayosisi mpya zimezaliwa maeneo yale yaliyokuwa misioni mfano **Dayosisi Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria**, **Dayosisi ya Kusini Mashariki**, **Dayosisi ya Ruvuma** na **Dayosisi ya Ziwa Tanganyika**. Umoja na uwajibikaji wa Wana-KKKT umewezesha dayosisi hizi mpya kuzaliwa na kuendelea kulea **maeneo ya misioni** valivobaki nchini: Kigoma Tabora na Zanzibar.

Kwa kawaida rangi ya shati la Mchungaji ni nyeusi. Katika mojawapo ya mikutano ya Wachungaji wote wa KKKT suala hili lilijadiliwa. Lakini inaelekea kwamba suala hili limekosa nguvu na ndio maana rangi za kila aina zimeendelea kuvaliwa na Wachungaji wetu. Ili kudumisha umoja na utambulisho wetu kama wana-KKKT tuisupuzie rangi ya mavazi ya kazi.

Ijapokuwa mazingira na jiografia za dayosisi zetu inatofautiana, lakini ipo haja ya KKKT kuweka utaratibusi wa jinsi ya kutunza watumishi wake waliokazini na wastaa ili kuwajibika na umoja wa kanisa letu uonekane kwa jinsi watumishi wanavyotunzwa kwa rasimilimali tulizopazo.

Kanisa litajahidi kutatua migogoro yake yenye kabla ya kuipeleka katika vyombo vy ya Serikali. Taratibu za kushughulikia migogoro hii ziwe za Kikristo. Mambo yakifika kwenye vyombo vy ya habari iwe kweli kanisa limeridhia.

Hitimisho: KKKT ni kanisa kubwa hapa Tanzania na Afrika, hiyo linaushawishi mkubwa kwa madhehebu mengine ya Kikristo. Jitihada zetu za kuimarisha umoja wetu kama viongozi kwanza na hatimaye katika kutekeleza yale yote tunayokubaliana litafisha nguvu za maadui wa ndani na nie ya kanisa.

Tuwe mfano kwa mengine kwa jinsi tunavyo shikamana na kuendesha shughuli za pamoja. Msemo kuwa: ‘umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu’ uendelee kutukumbusha juu ya wajibu wetu wa kutekeleza maamuzi na mapatano ya vikao vyetu mbalimbali.



Mwenyekiti wa LMC, Askofu Dkt. Israel-Peter Mwakyolile, ambaye pia ni Mkuu wa Dayosisi ya Konde akisalimu Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT.



Kamati ya Maandalizi ya Mkuu wa KKKT.

UMOJA NA UTAMBULISHO WETU KATIKA Kuabudu

Na Askofu Dkt. Owdenburg Moses Mdegella

UTANGULIZI

Kanisa lolote duniani lina **Ibada** na kila kitu kilicho ulimwenguni kina **utambulisho** wake. Mungu hulusiana na sisi kwa njia mbalimbali za utambulisho wetu. Nchi zote za dunia zinaitwa kwa jina la nchi au taifa husika kwa kuwa na utambulisho wa vitu kama bendera, wimbo wa taifa, pia tunu na mipaka ya taifa husika huheshimiwa na kulindwa. Vivyo hivyo, hakuna Kanisa linaloweza kuwepo, kukua na kustawi bila **umoja na bila utambulisho**.

Watangulizi wetu wa Karne ya 16 na 17 hawakuweka maungamo yetu kwa faida yao bali kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu. Waliopewa neema ya kutunga na kuandika nyimbo za kumwabudu na kumsifu Mungu kuanzia Karne ya 15 hadi ya 21 kwa ni kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Kwa umaja wake, taaluma na karama zilizo ndani ya Kanisa; limekuwa likipitia mara kwa mara kuhakikisha kwamba karama za Roho Mtakatifu kwa watu wa Mungu zinafanya kazi ndani ya Kanisa kwa njia ya Ibada.

Nadharia ya kuwepo kwa Kanisa haiwezekani bila kukusanyika. Kukusanyika hakuna maana bila kuwa na namna ya kuabudu pamoja. Kuabudu pamoja hakuwezekani bila misingi, mfumo, utaratibu na usahihi wa kinachofanyika. Hivi vyote hukamilishwa katika umaja. Haiwezekani kukawa na Ibada ya kweli kama kila mtu atafanya anavyotaka katika kusanyiko la watu wa Mungu.

Kanisa lenye mwelekeo wa Ibada zake huwa na liturgia lakini Kanisa lisilo na mwelekeo, ni sawa na meli au ndege isiyu na dira. Matendo yanayoambatana na kukusanyika pamoja kwa umaja ni kushirikiana katika Sakramenti za Ubatizo na Ushirika wa Meza ya Bwana kwa kufuata na kutii maagizo ya Bwana wetu Yesu Kristo kama yanavyofanuliwa na Neno la Mungu. Vivyo mifumo, misingi na njia za kujenga umaja katika Ibada huitwa LITURGIA.

Liturgia ni misingi bayana unaoweka waumini pamoja kwa UMOJA wa huduma ya Neno na Sakramenti vinavyo ambatana na mwitikio wa matoleo ya zaka, sadaka, shukrani, dhabihu na malimbuko kama kauli ya utii na furaha ya kupewa wokovu na Mungu. Liturgia ni kusema kwamba haiwezekani kumwabudu Mungu katika Roho na kweli pasipo umaja.

Misingi ya Kilutheri inayotokana na **Matengenezo ya Kanisa** ilikuja na Wamissionari wa Kijerumani, Kiswede, Kinorwjeni, Kifini, Kidenish na Kimarekani. Wamarekani walikuja pia na mapokeo ya Kilutheri kama yetu wakaongeza na mapokeo ya Waingereza hasa katika Nyimbo za Sifa. Huko ndiko tunakopata nyimbo kama za **Tenzi za Rohoni na Nyimbo za Injili**. Kila Kanisa limeongeza kwa wingi au kwa uchache mambo ya kuabudu yanayolingana na utamaduni/lughu za watu na jinsi Injili inavyotafsirika katika mazingira husika. Hii ndio sababu ya Kanisa letu kuwa na **Kamatyi ya Kitabu cha Tumwabudu Mungu Wetu** (TMW) na pia ni sababu moja wapo ya kuwa na **Kamatyi ya Theolojia na Maadili** (KATHEMA).

Hali iliyopo sasa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ni kwamba Kanisa linaabudu katika msambaratiko wa kukosa umaja na kupoteza utambulisho wake. Japo tuna kitabu kimoja cha umaja wetu cha TMW lakini Sharika nyingi hazitumii kitabu hiki ipasavyo. Zipo baadhi ya Sharika katika Dayosisi zetu ambapo Washarika huenda na vitabu

mnyama wala ndege? Limetoka wapi Kanisa ambalo lina tabia ya kinyonga au popo? Tukifika hapo inabidi tuhoji viongozi wa juu wako wapi na wanafanya nini kuhusu tazito hilo?

Kanisa la Kilutheri la Canada linaufafanuzi huu kuhusu Liturgia: 'Liturgia inatujengea



Viongozi wa KKKT wakiwa meza kuu.



Askofu Dkt. Owdenburg Moses Mdegella,
Mkuu wa Dayosisiya Iringa.

kanisani wakatoka navyo bila kuimba hata wimbo mmoja. Mahali pengine hata utaratibu wa ibada ulio katika kitabu hicho haufuatwi na liturgia hudharauliwa na kuitwa mapokeo yaliyopitwa na wakati.

Ingekuwa vema viongozi wa ibada watunze umaja wa Kanisa katika kuabudu kwa kufuata liturgia yetu na siyo kuwa chanzo cha kusambaratisha umaja huo. Inatia uchungu ukiingia kwenye baadhi ya Ibada zetu halafu unashindwa kujua kama ni Kanisa letu ama la Kipentekoste au la Kikarismatiki. Ibada zingine zinapanana kama mikutano ya Injili. Ukipiriki ibada hizo unashindwa kujua Kiongozi wa Ibada anatumia Kalenda au la? Unajiliza anajua maana na Majira ya Kanisa yaliyivo na umuhimu wa kumkuza msharika kiakili, kinafsi na kiroho? Unashindwa kujua kama anafahahamu kuwa kuna sababu ya Kanisa kutembea na Yesu mwaka mzima?

Unahoji pia kama kiongozi amejandaa kwa ibada au alishtukizwa tu? Mahali pengine unaona amekuwa kama padre wa kikatoliki na katika ibada hiyo hiyo amekuwa kama TB Joshua na baadaye kama manabii wa Kusini mwa Afrika na Nigeria. Haupiti muda unakuta amegeuka kuwa mhubiri wa hadhara wa Kimarekani, nk. Ni kanisa gani hilo ambalo si

umoja wa Kiroho katika maisha ya utendaji na sakramenti. Hakuna Uinjilisti bila umaja, hakuna misioni ya Kanisa bila umaja. Hakuna maisha ya kiroho pasipo ibada. Hakuna ibada bila liturgia na hakuna liturgia hai pasipo umaja.'

Ndiyo sababu KKKT imechagua Neno Kuu la Mkutano Mkuu wa 19 uliofanyika Agosti 2015 kuwa: "Jitahidi kuuhifadhi umaja wa Roho katika kifungo cha amani" (Efe 4:3). Umoja huo unajieleza katika kusifu, kuabudu na kuomba kwa kuongozwa na Neno la Mungu.

Umoja na utambulisho wetu uko katika urithi wetu wa Kiinjili kwa mrengu wa mafundisho ya Luther na Ungamo la Ausburg lisilobadilishi. Urithi wetu umepimwa kwa kina. Urithi wetu si wa kuuonea aibu. Una hadhi na heshima yake. Ni wajibu wa viongozi wa Kanisa kuanzia wazee wa Kanisa mpaka Askofu kuhakikisha kwamba tunatunza na kulinda urithi wetu. Urithi wetu unaanza na Mtakatifu Augustana aliyeanzisha Shirika la Agustino. Huo ndio Urithi wetu. Urithi wa watu wanaojikita kwenye usomi wa kina halafu wanahubiri na kufundisha.

Kama iliyovo katika ndoa na familia suala la Ulutheri liliasiisiwa na Mungu mwenyewe. Kwa mkazo wa Waaugustana, Kanisa linaanza kwenye umaja katika familia kisha unaingia kwenye jumuiya ya waamini. Ili kutimiza azma hiyo walihitaji kuwa na mfumo. Mfumo ukawa ni maafikiano ya namna ya kukusanya watu, hasa kuimba kwa sauti nne, kuhubiri na kuwaelekeza waumini na wasikilizaji kutoa zaka na sadaka kisha kuwataka wafike ibadani Jumapili kwa Huduma ya Neno na Sakramenti. Huo ndio mwanzo wa Urithi wetu wa Umoja na Utambulisho wetu kama Kanisa.

Makanisa mengine yana umaja katika liturgia yake kwa ajili ya ibada zake na makanisa mengine hayana umaja katika mfumo wa ibada zake. Kanisa letu lina liturgia moja ya umaja. Inabidi viongozi wa Ibada wajifunze vema mfumo wa ibada zetu. Umoja na utambulisho wetu katika kuabudu unaanza kwenye kumheshimu na kumwogopa Mungu na kumpenda ye ye Kuliko vitu vyote. Ibada za Kilutheri ni za Kibiblia. Ila zinawenza kubadilika kwa makubaliano si kwa kila mtu kufanya atakavyo.

UMOJA NA UTAMBULISHO WETU KATIKA Huduma ya Neno na Sakramenti

Na Mchg. Dkt. Anneth Munga

HUDUMA YA NENO KATIKA KKKT

"Tunaokolewa kwa Neema kwa Njia ya Imani katika Yesu Kristo!" Maana ya Ndani ya Imani ya Kanisa la kweli ni Yesu Kristo na kazi yake ya Ukombozi. Fundisho la msingi ni kwamba Wokovu unapatikana kwa Neema kwa njia ya Imani katika Yesu Kristo. Kategkisimo Ndogo aliyoiandika Martin Luther kufuatia uchungu alioupata alipoona wakristo wanapotoshwa kwa mafundisho potofu inasisitiza juu ya Neema.

Martin Luther alikuwa anapinga biashara ya barua za msamaha ambayo ilikuwa inafanyika katika kanisa. Luther alisimama imara akisisitiza kwamba Msamaha wa dhambi na Uzima wa ulimwengu ujao hauwezi kupatikana kwa fedha. Damu ya Ukombozi iliyomwagua msalabani ndio imeleta Neema na **Neema hiyo hainunuliki**. Inatosha na ndiyo peke yake inayoweza kuleta wokovu.

Hivyo Makanisa yanayounda KKKT yanatambulishwa na mafundisho yanayoweka mkazo katika Yesu Kristo na wokovu aliouleta kwa kufa msalabani.

Maandiko Matakatifu (Biblia) ndilo Neno la Mungu linalomfanya mwanadamu akutane na Mungu. Maandiko Matakatifu ni Neno la Mungu kwa sababu ni Ushuhuda wa Mitume waliomfuta Yesu Kristo. Pamoja na Maandiko Matakatifu, Kiri za Imani ni za Msingi katika Maisha ya Mkristo na maisha ya Kanisa kwa sababu zimetengenezwa ili mtu abadilike kabisa kutoka kwenye njia ya uovo, na mabadiliko hayo yaonekane na yawe ya kudumu. Kwa sababu hiyo, Luther alikaza kuwa lazima wale wanaohubiri wawe ni wacha Mungu.

Martin Luther alikuwa Profesa lakini usomi haukumfanya adharau nafasi ya kutafakari kiroho. Ni wazi kwamba mikazo ya Martin Luther ilikuwa kichocheo hata kwa watheolojia waliomfuta baadaye kama akina Francke na Zinzendorf walioweka misingi ya kilichoitwa theolojia ya moyo, wakisitiza kwamba kusoma Maandiko hakutakiwi kuwa zoezi la kiakili peke yake.

Kwa hiyo hata wanafunzi wa Theolojia wanapojifunza Kiyunani, Kiebrania na Kilatini; lugha zinazowawezesha kusoma Biblia Hebraica, Septuaginta, Agano Jipyia la Kiyunani, Vulgata, na tafsiri za nyakati mbalimbali za Maandiko Matakatifu, ujuzi huo hautakiwi tu kuwafanya wawe mahiri katika kuchambua Maandiko Matakatifu bali wanawezeshwa kusikiliza na kufahamu kwa undani ujumbe uliomo kwenye Maandiko hayo kwa faida yao wenyewe. Hapo ndipo watakapeza kuliwakilisha Neno la Mungu kwa watu.

Kuhubiri ni kufundisha, kwa hiyo ni wajibu wa wale waliopewa Huduma ya Neno kuhakikisha kwamba watu wanaosikiliza wanaelewa. Katika kusitisitza hili, Martin Luther alisema: "...wahubiri waangalie vizuri kwamba, wasizifundishe kwa njia tofauti Amri Kumi za Mungu au Sala ya Bwana au Ukiri wa Mitume au Sakramenti

mara kwa mara. Badala yake watumie daima mfano uelele wanapofundisha na wanapoeleza umati. Ninataka kilitoa shauri hilo kwa sababu ya kujua kwamba, si rahisi kuwafundisha watu wasio wasomi sana au vijana, tusipotumia tena na tena mfano uelele wa maneno.... Hatuna budi kuwafundisha wale wasio wasomi sana na vijana bila kuibadilisha silabi hata moja wakati wowote wa mafundisho ili muundo wa kazi hii uwe ni uelele daima."

Inaweza ikaonekana kana kwamba Professor Martin Luther alikuwa anadharau watu wasiokuwa wasomi. Lakini maana yake haikuwa kudharau au kudhalilisha au kubea kundi la watu bali katika kuweka msisitizo huu anaweka wajibu wa kufikisha ujumbe kwa wale



**Mchg. Dkt. Anneth Munga,
Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu
ya Sebastian Kolowa (SEKOMU).**

waliopewa wajibu wa Huduma ya Neno. Hiyo ni sehemu muhimu ya utambulisho wetu kama KKKT.

Tunazo taratibu za Mafundisho na Malezi katika ngazi mbalimbali watekelezaji wakiwa sio tu Wachungaji bali pia Mashemasi, 'Parish Workers', Waalimu wa Elimu ya Kikristo na Wainjili. Hawa wameandalishi na wanapaswa kujua kuwa kila mtu ana haki ya kulipata Neno na kwa hiyo wafanye jithihad stahiki za kumfikishia msikilizaji Neno kwa namna alivyo na anavyoweza kulipokea.

Katiba ya KKKT na Katiba za Dayosisi za KKKT zinaweka msingi wa Utaratibu wa Utoaji wa Huduma ya Neno na Sakramenti. Wasimamizi wa Huduma hii ni wanaume, na kuanzia mwaka 1991, na wanawake, walioandalishi na kubarikiwa kuwa wachungaji kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Miaka 30 iliyopita, Chuo cha Theolojia cha Kilutheri Makumira palikuwa panabubujika kwa mijadala ya waliokuwa wanaunga mkono au kupinga suala la wanawake kubarikiwa kuwa Wachungaji. Inafurahisha kuona kwamba sasa tunafikia mwaka wa 25 tangu wanawake washirikishwe katika Huduma ya Uchungaji.

Maandalizi ya wahudumu wa Neno na Sakramenti katika KKKT yamekuwa yakifanywa Makumira (ambapo sasa ni Chuo Kikuu). Tangu ianzishwe, taasisi hii imetoa Elimu ya Theolojia na Masomo ya Kichungaji kwa wanafunzi wanaotumika. Kwa nyakati mbalimbali, Mwika, Ruhija na Chuo Kikuu kishiriki Iringa pia

zimetoa Elimu ya Theolojia. Baadhi ya Dayosisi zinatoa mafunzo ya kuanda Wachungaji wake. Mojawapo ni Dayosisi ya Kaskazini Mashariki. Asilimia 100 ya wahadhiri wanaofundisha masomo ya Theolojia katika program hiyo ni matunda ya Makumira kwa maana kwamba mafunzo ya msingi katika Theolojia waliyapata Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, jambo ambalo linaufanya utambulisho na umaja wetu kupanuka na kuwa endelevu.

**UTAMBULISHO WETU KATIKA HU
YA SAKRAMENTI:** Chakula cha Bwana au Karamu ya Madhababu inajengwa juu ya agizo la Yesu Kristo alilotoa wakati wa karamu yake ya mwisho na wanafunzi wake. Maneno muhimu ni yale yanayosemwa wakati wa kufanya magawanyo: 'Pokea mwili wa Bwana wetu Yesu Kristo; Pokea damu ya Bwana wetu Yesu Kristo'. Ingeefaa kila mshiriki asikie maneno yote na siyo sehemu tu kwa kigezo kwamba muda hautoshi au kwamba watu ni wengi.

Katika miaka ya 1970, kushiriki Chakula Cha Bwana (CCB) ilikuwa ni tendo lilioluwa likingojewa kwa hamu na kwa heshima kubwa. Ikitangazwa kwamba mwisho wa mwezi huu kutakuwa na CCB, washarika wanakuwa katika kuonyesha subira.

Katika Usharika wangu wa Mafinga Lutheran Training Centre, CCB ilikuwa inatangazwa mapema ili watakaoshiriki wajandikishe. Siku ya CCB ikifika, tulikuwa kwanza tunahudhuria Ibada ya kawaida ya Siku ya Bwana mpaka hatua ya kutoka nje. Baada ya hapo ndipo wale waliojandikisha wanaingia tena kanisani kwa ajili ya CCB.

Hata kama washarika hatukuelewa kwa undani fundisho la 'Consubstantiation', ule upekee uliotokana na CCB kutangazwa mapema, kuijandikisha, kuingia wenyewe kanisani baada ya Ibada ya Siku ya Bwana ulikuza hisia za kuona kuwa CCB ni jambo la kimiujiza na sio kitu cha kawaida.

Tamaduni zetu pia zinazohusiana na nyakati maalum zinatumika kuipa CCB hadhi ya ziada. (k.m. Usambara: Wanawake kutofunika vichwa kama ishara ya heshima). Martin Luther aliweza kutaja mambo ambayo yangemfanya mtu asistahili kushiriki Chakula cha Bwana. Na Dayosisi zote za KKKT zina utaratibu wa Marudi kwa mujibu wa Katiba zao.

MAPENDEKEZO:

UNGAMO LA DHAMBI NA MSAMAHNA: Maeneo haya ya Litrurjia yasifanywe tu kwa mazoea bali yawe pia sehemu ya mafundisho katika vikundi au sharikani kwa ujumla kama zinavyofanyika semina za uwakili, maisha ya ndoa, na nyingezeo.

UBATIZO WA WATOTO wadogo upewe uzito na lifanyike kwa namna itakayofundisha umuhimu wake.

**MALEZI KWA NJIA YA HU
KWA WATOTO:** Mafundisho ya watoto, vijana na wanafunzi yapewe kipaumbele kwa maana ya vitendea kazi, muda na ufundishaji jumuishi. Watoto sio kanisa la kesho. Watoto ni sehemu ilioyai hai na muhimu ya Kanisa la leo.

MITAALA YA VYUO vinavyofundisha theolojia viingize masomo ya msingi ya Lughya Alama kwa ajili ya kuweza kutoa Huduma ya Neno na Ushauri Kichungaji. Lughya Alama sio tu kwa ajili ya viziwi peke yao bali ni "supportive non-verbal language" inayomsaidia mtu yeoyote.



KKKT ni moja ya makanisa makubwa duniani

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ni moja ya makanisa makubwa duniani hivyo maamuzi katika vikao vyake hufuatiliwa na makanisa mengine duniani.

Hayo yalismwa na Mch. Dkt. Elieshi Mungure, Katibu wa Afrika Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) akimpa Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa zawadi kutoka Fungamano hilo mara baada ya Dkt. Mungure kuusalimu Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT. Askofu Dkt. Malasusa pia ni Makamu wa Rais FMKD Kanda ya Afrika.

ifanyike 2017 isemayo: '*Umoja na Utambulisho wa Kanisa la Kilutheri*'.

Kwa upande wake Mch. Dkt. Anneth Munga akitoa mada kuhusu *Umoja na Utambulisho wetu katika Huduma ya Neno na Sakramenti*, alisema "KKKT inakua kwa marefu, kwa mapana na kwa kina. "Kwa marefu; kwa maana kila siku, juma, mwezi na mwaka unaopita, Kanisa hili linakua kiumri, na hivi sasa limetimiza miaka 52. "Kukua kwa mapana, kunajidhihirisha kwa uwepo

wa maeneo ya Misioni ndani na nje ya Tanzania. Kukua kwa kina kunajionyesha katika ongezeko la idadi ya Wakristo.

Kwa mujibu wa takwimu zinazonyeshwa kwenye Taarifa ya Mkuu wa Kanisa, wakristo wa KKKT wameongezeka kutoka 5,600,000 kwa mwaka 2011 hadi 6,531,336 kwa mwaka 2014, yaani wakristo 931,336. "Ongezeko hilo linawenza kulinganishwa na jumla ya idadi ya washarika wa Dayosisi za Dodoma (19,376) Dayosisi ya Kusini (190,105), Dayosisi ya Kusini Magharibi (28,000), Dayosisi ya Kaskazini (324,562), Dayosisi ya Meru (89,116), Dayosisi ya Mbulu (81,990), Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria (18,707) na Dayosisi ya Karagwe (176,502) kwa pamoja (Jumla 928,358). "Kwa vyovyote, moja ya sababu za ongezeko la jinsi hii ni *Maisha ya Ushuhuda ya Kanisa letu*. Kwa ukuaji wa jinsi hii, huduma ya Neno na Sakramenti inahitaji kuwa imara wakati wote ili Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania liendelee kuwa Kanisa lenye ushuhuda kwa mwenendo na maisha yake halisi na sio kwa jina tu", Dkt Munga alisema.



Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa akihubiri wakati wa Ibada ya Ufunguzi wa Mkutano Mkuu.



Askofu Mstaafu Profesa Hance O. Mwakabana aliongoza Somo la Biblia kutoikana na Neno Kuu: "*Jitahidi kuuhihadhi Umoja wa roho katika kifungo cha Amani*" (Efeso 4: 3)



Mch. Luke Mwololo Katibu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Kenya (KELC) alitoa salamu na kuomba wajumbe waombe kwa ajili ya amani kutoikana na tishio la ugaidi Afrika Mashariki.



Picha ya kumbukumbu: Mch. Dkt. Elieshi Mungure (Dawati la Afrika FMKD); Bibi Alice Mtui (Mwandishi); Askofu Dkt. Fredrick Shoo (aliyechaguliwa kuwa Mkuu mpya wa KKKT); Askofu Dkt. Alex Gehaz Malasusa (Mkuu wa KKKT anayemaliza muda wake); Bw. Brighton Killewa (Katibu Mkuu wa KKKT) na Bw. Loata Mungaya (Naibu Katibu Mkuu Fedha na Utawala KKKT).

Na Elizabeth Lobulu

Wakati wa Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT uliofanyika Agosti 2015, uliandaliwa mdahalo kuhusu **Umoja na Utambulisho wa KKKT**. Haya ni baadhi ya mambo yaliyojitekeza:

Mchg. Dkt. Rose Materu (Mtoa mada), alishauri Wachungaji wasinyamaze wanapoona taratibu ngeni zikipenyezwa wakati wa Ibada bali inafaa wasimame katika nafasi zao na kutoa mafundisho sahihi kwa Washarika katika ngazi mbalimbali.

Askofu Profesa Hance Mwakabana (aliyefundisha Somo la Biblia) alisema Katiba ya KKKT inatoa wajibu wa Mchungaji kwamba ni kufundisha na ni sehemu ya kiapo cha Uchungaji KKKT. Alisema upo umuhimu wa Viongozi wa Sharika kutawala madhabahu.

Askofu Dkt. Owdenburg Mdegella (Mtoa mada), alishauri utaratibu wa Ibada wa KKKT ufuatwe na kwamba nyimbo toka Kitabu cha Tumwabudu Mungu Wetu (TMW) zitumike Ibadani.

Alikemea tabia ya kuingiza mapambio badala ya kufuata utaratibu wa Ibada na nyimbo za majira ya Kanisa. Alisema kama kuna Viongozi wa Ibada

Mdahalo wavutia wajumbe



Mchg. Profesa Joseph Parsalaw Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira akichangia katika mdahalo. Askofu Dkt. Steven Munga (watatu kutoka kushoto na katika picha ndogo juu) alikuwa Mwenyekiti wa jopo la mdahalo.



Kwaya kutoka Dayosisi ya Iringa.



Wajumbe wakimpongeza Mkuu mpya wa KKKT Askofu Dkt. Frederick Shoo.



Askofu Emmanuel Makala akiwa katika Mkutano Mkuu wa 19 wa KKKT.

wasiofua taratibu zilizowekwa kwa pamoja KKKT; Maaskofu watoe waraka kuwakumbusha wahusika na inapobidi waombe viongozi wengine wasaidie endapo tatizo ni kwa sababu tu ya ugumu wa miyo ya wanaoongoza.

Wakichangia baadhi ya wajumbe walitaka mitaala ya kuandaa Wachungaji ipitiwe upya na kuiimarisha ili mafunzo yasaidie kuondokana na shida ya Wakristo kuyumbishwa na mafundisho

potofu hasa kuhusu kuabudu, kutubu, kufanya maombi, kutoa sadaka na matumizi ya liturjia ya KKKT katika Ibada.

Mchg. Dkt. Elieshi Mungure alisisitiza kuwa hakuna budi kwa kila Msharika kujitathmini kwamba je kuwa Mlutheri ina maana gani na tofauti yake na muumini wa madhehebu au kanisa jingine?

Mchg. Dkt. Anneth Munga (Mtoa mada), alitoa wito kwa wachungaji kuwa

wacha Mungu; kusoma vizuri Neno la Mungu; na kuhakikisha wanajianaa vizuri kwa ajili ya Ibada ya Siku ya Bwana, nk.

Maandalizi ni pamoja na kupanga ushiriki wa kwaya na hata kijiandaa kwa nyimbo za TMW zitakazotumika. Alitaka Kanisa liandae walimu wa Elimu ya Kikristo na watoto waweze kufundishwa wangali wadogo ili wasiyumbishwe na mafundisho potofu.

Inatupasa kuwatetea watoto kwa kulinda haki zao kwa vitendo na sio kwa maneno tu.

MTOTO NI NANI? Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009; mtoto ni mtu aliye chini ya miaka 18. Watoto wanaathiriwa na udhalilishaji ambao waweza kuwa wa kiuchumi, kimapenzi, ubaguzi wa kijinsia, elimu na huduma za afya. Miongozo ya Kimataifa ikiwemo mikataba, sheria na matamko mbalimbali inaonyesha viwango vinavyojulikana kama 'Haki za Binadamu' zinazotakiwa zitekelezwe na Serikali na wanaohusika wote wanaowajibika kulea na kutunza watoto.

Viwango hivyo vinapaswa kuheshimu utu wa kila binadamu bila kujali rangi, jinsi, lugha, dini, mitazamo, asili, utajiri, hali ya kuzaliwa au uwezo wa mtu yeyote. Viwango hivi vinategemeana na havigawanyiki na vinatoa majukumu kwa serikali, wadau wengine, na mtu mmoja mmoja kuhusiana na haki za watu wengine. Sheria zilizowekwa na Mkataba wa kimataifa juu ya Haki za Binadamu zinatumika kwa wote kuanzia watoto hadi watu wazima. Na watoto wanatajwa kwa upekee kwenye Mkataba wa Haki za Binadamu.

HALI HALISI: Watoto wanakatiliwa haki zao kuanzia ngazi ya familia, jamii na taifa kwa ujumla katika nyanja mbalimbali za maisha; wengi wao hukatiliwa haki zao na wazazi, walezi, ndugu wa karibu au watu wanaowazunguka mahali wanapoishi.

Baadhi hutenda ukatili kwa watoto kwa kutokujua kutohana na majeraha katika nafsi zao kwa kuwa wao waliteswa utotoni. Wengine huwakatili kwa kudhamiria kwa mfano watoto wengi waliozaliwa nje ya ndoa hawatambulishwi baba zao, wengine hupewa majina mabaya kama: 'Sipendeki', 'Sijali', 'Shida', 'Tabu', n.k.

Vilevile watoto walemau hubaguliwa kutokana na hali zao kwa kufungiwa ndani, kutoshirikishwa katika maamuzi hasa katika familia zilizo nyangi, kubaguliwa kwa kuzingatia hali zao za vipato na walio yatima hunyimwa hata kutumia rasilimali za wazazi wao kuijendezeza.

NDOA KUVUNJIIKA: Baadhi ya ndoa zimevunjika kwa sababu ya mafundisho hafifu wanayopewa wanandoa kuhusu malezi ya watoto na jinsi ya kutunza ndoa au kufundishwa kwa muda mfupi sana kabla ya kuoana. Hali hiyo huweza kusababisha migogoro na magomvi katika familia na huathiri watoto na vitendo yva ukiukaji wa haki za watoto kutokea.

MILA POTOFU: Pia zipo mila na desturi mbalimbali zinazokiuka haki za

Tubadilike tuondoe ukatili dhidi ya watoto

watoto. Mila hizo potofu ni kama ukeketaji wa watoto wa kike na ndoa za utotoni kwa kuoza mabinti wadogo kwa lazima.

WAZAZI NA WALEZI: Katika kuhakikisha ustawi wa watoto wazazi wanawajibu kutunza watoto wao kwa kuwapa elimu; mapumziko; wakicheza wafuatilie wanacheza wapi, na nani na wanacheza nini? Wajibu mwagine ni kulinda watoto kwa kuhakikisha kwamba wazazi wakiwa hawapo watoto wanabaki na walezi (sio kuwapa dawa za usingizi).



yake kwa ujumla.

Si kila kazi inayofanywa na mtoto, chini ya umri wa miaka 18 itachukukuliwa kama ajira kwa watoto. Kuna mamiloni ya watoto wanaofanya kazi zinazoendana na umri wao na jinsi walivyopevuka. Kwa kufanya hivyo watoto hao hujifunza mambo mengi kama vile kuwajibika kwa jamii, kupata ujuzi, kujifunza njia za kujiongezea kipato na kuinua pato la taifa, hili halitachukuliwa kama ajira kwa watoto.

AJIRA KWA WATOTO: Mambo yanayosababisha kuwepo ajira kwa watoto ni umaskini; migogoro ya kifamilia; ukosefu wa elimu kwa wazazi na uhitaji wa kipato; ajira zenye ujira mdogo; ukosefu wa elimu na fursa; ujinga yaani kutoelewa mahitaji muhimu kwa watoto na shughuli za kimila/ kijadi.

MADHARA YA AJIRA: Madhara yanayoletwa na ajira kwa watoto ni kama vile umaskini; udhalilishaji kisaikoloja – kumnyang'anya utoto wake; kukoma maipemba kiakili, kifirka, kihisia na kudhurika kiafya na huweza kupata maambukizi ya Virusi nya UKIMWI (VVU), nk.

HITIMISHO: Watoto ni zawadi toka kwa Mungu. Watoto ni baraka. Mungu anaweza kuwatumia watoto kutubarki, kururudi katika kusudi la awali la Mungu aililotuamini sisi watumishi katika UWAKILI wa UUMBAJI ili tuweze kuwatunza, kuwalea, kuwafundisha na kuhakikisha ustawi wa watoto katika familia, kanisa na jamii. Watoto wamekosa misingi ya mafundisho kutokana na UTANDAWAZI na uhuru wa kupita kiasi. Hivyo TUBADILIKE, TUPAMBANE NA UKATILI DHIDI YA HAKI ZA WATOTO KATIKA JAMII. "Hazina za uovu hazifaidii kitu, bali haki huokoa na mauti. BWANA hataicha nafsi ya mwenye haki ife na njaa; Bali tamaa ya mtu mwovu huisukumia mbali" (Mithali 10: 2-3).



Bibi, Faustina Nillan Losai
Mkurugenzi wa Wanawake na Watoto KKKT.

AJIRA KWA WATOTO: Ajira kwa watoto inaweza kutafsiriwa kama kazi yoyote inayoweza kufanya na mtoto chini ya umri unaotambuliwa kisheria. Ajira za watoto ni vitendo au kazi za kiuchumi au zisizo za kiuchumi, zinazofanywa na mtoto ambazo zinaweza kuhatarisha maisha yake, afya yake, elimu yake, utu wake na maendeleo

(Wasiliana na Faustina Nillan kwa sms: 0767823144)

Ziara ya Kwaya ya Vijana Bukombe

Kwaya ya Uinjilisti ya Vijana ya Usharika wa Arusha Mjini, ilifanya ziara ya Uinjilisti Dayosisi Mashariki ya Ziwa Victoria (DMZV) katika Kijiji cha Nampalahala Wilaya ya Bukombe.

Wanakwaya hao 41 walifanya ziara 25 Julai hadi 2 Agosti 2015 kwa mwaliko wa **Timu ya Askofu Andrew Gulle na Wahubiri (ASWA)**

ya DMZV. Katika ziara hiyo, "**Timu ya ASWA**" na wanakwaya hao toka Arusha waliunganisha nguvu na kufaulu kusimamisha nguzo na kuezeka paa la **Nyumba ya Ibada** Kijijini Nampalahala na Dayosisi ilimteua Mwinjilisti Richard Mdoe ili aendelee kutoa huduma kijijini hapo.

Saa za asubuhi timu hizo zilikuwa zinafanya Uinjilisti **Nyumba kwa Nyumba**. Na jioni wagonjwa waliombewa katika **Mikutano ya Injili** iliyokuwa ikifanyika eneo la Sentani na kuhudhuriwa na watu 300 kila siku. Matunda yanaonekana kwani kila Jumapili kati ya watu 350 hadi 400 wameanza kuhudhuria Ibada Jumapili. Kijiji kina wakazi 1,000. Kwa sasa kwaya 23 ya Vijana na ya Watu wazima zimeanzishwa.



Kwaya ya Uinjilisti ya Vijana ilipofanya ziara Kijiji cha Nampalahala kilomita 60 toka Geita kwa mwaliko wa DMZV.



Wanakwaya waliungana na timu ya Askofu Andrew Gulle ASWA kufanya mikutano ya Injili kila jioni.



MwenyeKITI wa Kwaya ya Uinjilisti ya Vijana KKKT Usharika wa Arusha Mjini, Bw. Felix Mwetha, akiwa na mtoto mdogo ambaye alikuwa na hirizi mbili shingoni: moja iko kwa mbele na nyingine kubwa iko mgongoni. DVD ya Ziara hiyo inapatika sasa, **Mawasiliano:** <uinjilistikwaya@yahoo.com> au <mwethaf@yahoo.com>



Mikutano wa Injili katika Kijiji cha Nampalahala Sentani ilihudhuriwa na watu 300 kwa siku.



Je wewe kama mwanajamii; siku hiyo imekukumbusha kutambua njia nzuri ya kumsaidia mtoto wa kike?

Katika maeneo mengi kutokana na ugumu wa maisha watoto wa kike huchukuliwa toka nyumbani kuwa 'mahausigeli' hasa mijini lakini watoto kama hawa hawatendewi haki.

Baadhi hutumika kama watumwa. Hutendewa ukatili kama kupigwa na kuunguzwa kwa pasi ya moto au kuchomwa visu bila sababu.


Jamii kwa jumla ichukue hatua kukomesha ukatili katika kwa watoto wa kike.

Mtoto wa kike alindwe na kupewa haki


Umoja wa Mataifa umetangaza tarehe 11 Oktoba kuwa siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike.

Ni siku ya kutafuta fursa kuwaendeleza watoto wasichana na kuwaangaliza watu waone ubaguzi kwa watoto wasichana duniani.

Watoto wa kike hunyimwa fursa ya elimu, haki za kisheria, lishe, matibabu na ulinzi dhidi ya ubaguzi, ukatili na baadhi kulazimishwa kuolewa katika umri mdogo.



Watakatifu ni pamoja na wanaomtumikia Bwana



Na Mch. Profesa Gwakisa E. Mwakagali

Kwa kufuata Kalenda ya Biblia ya KKKT, Siku ya Watakatifu inaadhimishwa Jumapili ya kwanza ya Novemba kila mwaka. Mwaka 2015 iliadhimishwa Novemba Mosi.

KANISA LA MWANZO

Swali linalojiteza hapa ni: Hao Watakatifu ni akina nani? Na kwa nini wanakumbukwa? Dini nyingi zilizopo ulimwenguni zina watakatifu wao wanaokumbukwa na kuheshimiwa na hata kuabudiwa. Wabuda na Wahindu wana watakatifu wao. Katika Kanisa la kwanza (The Early Church) lilifundisha: "Wakristo waaminifu katika ulimwengu huu walikuwa sehemu ya *Ushirika wa Watakatifu*".

KANISA KATOLIKI

Katika imani ya Kanisa Katoliki 'Mtakatifu' ni mtu yeoyote aliyetangazwa rasmi na kanisa kwamba ni Mtakatifu na anaaminika kuwa yuko mbinguni hivyo anapaswa kuheshimiwa (venerate) na wakristo na kanisa kwa ujumla (siyo kuabudiwa). Watakatifu hao wanakumbukwa kwa kuigwa mfano wa maisha ya uaminifu na uchaji kwa Mungu.

Ni imani ya Kanisa katoliki kwamba watakatifu wanauwezo wa kuwaombea wakristo kwa Mungu na baadhi ya Watakatifu wanahesabiwa kuwa walini wa wakristo walio hai. Kati ya watakatifu wanaotambulika na Kanisa Katoliki ni pamoja na Mariamu mama yake Yesu ambaye anaitwa 'Mama Mtakatifu' na 'Mama wa Mungu'. Na Papa anaitwa Baba Makatifu kwa kuwa ni mrithi wa kiti cha Mtume Petro Mtakatifu na mwakilishi wa Kristo ulimwenguni.

KANISA LA KIINJILI

Kwa Walutheri na makanisa yenye mfumo wa Kiinjili, watakatifu ni

wanadamu wenye dhambi wanaostahili msamaha wa dhambi zao. Kufuata imani ya Kilutheri haijaandikwa popote katika Maandiko Matakatifu (Biblia) kwamba tunapaswa kuwaomba ama kutafuta msaada wa kiroho kutoka watakatifu.

Wala haijaandikwa lolote kuhusu kuwaomba watuombee kwa Mungu, kufunga kwa ajili yao wala kuadhimisha sikukuu kwa ajili ya kila mmoja wao kama wafanyakyo wenzetu wakatoliki na makanisa mengine ya Ulaya; wala kutoa sadaka kwa ajili yao na wala kuanzisha huduma yoyote kwa ajili yao. Mambo hayo yangekuwa ni sawa na kuabudu sanamu (idolatry).

Maana ya watakatifu kwa Kanisa la Kilutheri ni wale wote wanaoshiriki kuitangaza Injili ya Kristo na kufundisha kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu.

Katika jumuiya hiyo wako walioitangulia (walio kufa) na wako walio hai. Hiyo ndiyo maana ya maneno: '*Ushirika wa Watakatifu*' katika Ukiri wa Imani ya Mitume.

Pia Watakatifu ni wale wote wanaomwamini Bwana wetu Yesu Kristo, yaani 'waaminio' wote.

Katika Biblia tunasoma Anania anavyosema "Bwana nimesikia habari za mtu huyu ... alivyowatenda 'Watakatifu' wako Yerusalem" (Mdo 9: 13, 32, 41; Mdo 26: 10). Mtume Paulo aliwaita Wakristo wa Usharika wa Rumi: "Wapendwao na Mungu, walioitwa kuwa 'watakatifu' maana imewapendeza watu wa Makedonia na Akaya kufanya changizo kwa ajili ya 'watakatifu' huko Yerusalem walio maskini" (Warumi 15: 25 - 26).

Paulo aliwaita wakristo wa Korintho: "...Wale walioitakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe 'watakatifu' pamoja na wote wanaoliitia jina la

Bwana wetu Yesu Kristo" (1Kor 1: 2). Paulo anawataka wakristo kushtakiana mbele ya 'watakatifu' na siyo mbele ya wasio haki kwa maana watakatifu watauhukumu ulimwengu (1Kor 6: 1 - 2). Katika Ufunuo Yohana anaeleza kuwa maombi ya 'watakatifu' ni manukato (Ufunuo 5: 8).

HITIMISHO

Makanisa ya Kiprotstanti huadhimisha Sikukuu ya Watakatifu ili kuwakumbuka waliomwamini Bwana Yesu Kristo, wakaitangaza *Habari Njema* ya Wokovu katika jina lake na kuishi maisha ya uaminifu na uchaji na kumpendeza Mungu. Kati yao wamo Mitume na wale Mashahidi wa maisha na kazi ya Yesu Kristo hapa duniani. Wamo pia watumishi wa Mungu ngazi mbalimbali walioitenda kazi yake kwa uaminifu na walioishi maisha ya kumpendeza Mungu na kuwa mfano wa kuigwa katika ulimwengu. Katika hao wamo wazee, wainjilisti, wachungaji, maaskofu na watumishi mbalimbali katika kanisa.


Wamo pia wakristo raia walioishi maisha ya uaminifu na uchaji wakawa mfano wa kuigwa katika jamaa zao, jamii na ulimwengu kwa jumla. Wengi wao wamelala mauti wakingoja siku ya kuja kwa Bwana wetu katika utukufu. Pia tumo sisi tulio hai wakati huu tukiendelea kumtumikia Bwana kwa njia mbalimbali na kuishi kwa uaminifu na uchaji katika ulimwengu wa sasa hadi Kristo atakaporudi.

Sikukuu ya Watakatifu pia itukumbushe juu ya uenyeji wetu wa mbinguni. Bwana akubariki mpendwa msomaji wa makala haya!

Profesa Mwakagali ni Mhadhiri mstaafu katika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira. Anapatikana sms: 0784 431 343 au 0715 932 806



Makanisa ya Kiprotstanti huadhimisha Sikukuu ya Watakatifu ili kuwakumbuka waliomwamini Bwana Yesu Kristo, wakaitangaza *Habari Njema* ya Wokovu katika jina lake na kuishi maisha ya uaminifu, uchaji na kumpendeza Mungu.



Ibada kwa lugha ya alama

Mchq. Enock Meas wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini akihubiri kwa kutumia 'lugha ya alama' hivi karibuni Usharika Mdogo katika Kituo cha Umoja Hosteli, Moshi. Mawasiliano yote tangu mwanzo hadi mwisho wa ibada hiyo Mchungaji hawaonegei kwa sauti na washarika nao hujibu kwa lugha ya alama tu.



Washarika wakimsifu Mungu kwa 'lugha ya alama' katika Usharika Mdogo Kituo cha Hosteli ya Umoja, mjini Moshi. Inabidi mgeni awe na mkalimani ili aleewe 'kinachosemwa'. Mwimba Zaburi anasema 'kila pumzi na imsisu Mungu' na ndio maana hata kwa lugha ya alama Mungu anaabudiwa. Sote tugaswe kuunga mkono huduma kama hii iwafikie walemaavu wengine.



Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo KKKT (mwenye miwani) akiwa katika picha ya pamoja na Washarika watumiao 'lugha ya alama' (bubu) mara baada ya Ibada ya Novemba Mosi 2015 mjini Moshi. Usharika unahudhuriwa na walemaavu wapatao 40.

Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo KKKT, Bw. M. W. Mallumbo, pamoja na Mchq. Thomas Maumbuka (katikati) kutoka Idara ya Mipango ya KKKT wakikabidhi zawadi ya vitabu 20 vya Tumwabudu Mungu Wetu kwa washarika wenyewe ulemavu (bubu) Usharika wa Mdogo wa Kituo cha Umoja Hosteli, mjini Moshi. Tendo hili liliifanyika tarehe 1 Novemba 2015.



Kwaya toka Dayosisi ya Ziwa Tanganyika yafanya ziara



Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, akiwa na Ujumbe wa watu 35 Wanakwaya ya Ebeneza kutoka Dayosisi ya Ziwa Tanganyika walipotembelea Ofisi Kuu ya KKKT, Arusha. Pamoja na mambo mengine walishiriki Ibada ya Asubuhi na kuimba nyimbo zilizovutia waliokuwa katika Ibada 23 Nov 2015.



Nyimbo za Kwaya hiyo zilimgusa Katibu Mkuu ambaye alianzisha harambee ya papo hapo kusaidia kwaya hiyo ambayo ilialikwa na Kwaya ya Uinjilisti ya Vijana ya Usharika wa Arusha Mjini, Dayosisi ya Kaskazini Kati. Kwaya hiyo ilipanga kufika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira na Dayosisi ya Kaskazini.

EVANGELICAL LUTHERAN CHURCH IN TANZANIA

JOB VACANCY

The Evangelical Lutheran Church in Tanzania, (ELCT), invites applications from qualified and experienced individuals for a vacant post of a **COMMUNICATION SPECIALIST**.

SUMMARY

To enlarge the Communication Desk, Church's website, news writing, editing and distribute a print magazine as well as to build and sustain relationships with the public and mass media on behalf of ELCT.

TERMS OF SERVICE

He/She will be appointed on a three (3) years contract basis renewable.

1. GENERAL REGULATIONS

- i. The applicant should be a Christian - Lutheran with not more than 35 years of age.
- ii. The applicant must attach his/her birth certificate.
- iii. The applicant should attach his/her curriculum vitae (CV), copies of academic certificates and three trusted referees.
- iv. The application should be signed by his/her Parish Pastor and a Diocesan General Secretary.

2. ESSENTIAL DUTIES AND RESPONSIBILITIES

- i. To enlarge communication department of the Church.
- ii. Responsible for coordinating the communications within the Church.
- iii. Produce, proofreads and maintains accurate communication content in the website.
- iv. Produces and distributes press releases.
- v. To manage press conferences.
- vi. To create and maintain positive relationships between media and other institutions.
- vii. Produce, organize and manage church events.
- viii To produce, edit and announce daily news to the website, blog and other social media.

3. QUALIFICATIONS AND SKILLS REQUIRED

- i. Applicant must be a Holder of a Bachelor's degree in Journalism or Communications from any recognized institution.
- ii. Must have at least three years of work experience in journalism or public relations duties.
- iii. Must possess outstanding written and oral communication skills.
- iv. Must be able to read and comprehend sometimes - complex instructions, sometimes - lengthy correspondence and memos.
- v. Must be able to write articles, editing and distribute print magazine.
- vi. Must be able to apply common sense understanding to carry out detailed issues of the Church.
- vii. Must be able to effectively present information in one-on-one and large group situations to people and organizations, senior management and other employees of the Church.
- viii. Must be able to plan and prioritize effectively.

4. COMPUTER SKILLS

Must possess good computer knowledge and skills such as competency in MS Office, E-mail and Internet browsing, Database software.

5. WORK ENVIRONMENT

Normal office environment.

6. SALARY

As per ELCT Common Work salary scales.

7. MODE OF APPLICATION

All applicants should be addressed to the Secretary General of the Evangelical Lutheran in Tanzania, (ELCT), P. O. Box 3033, Arusha, Tanzania. All applications should reach the office not later than 31 December, 2015.

Moshi Lutheran

Printing Press



Tunachapisha:

Vitabu vya aina zote
Majarida na Magazeti
Hati za Fedha
Madaftari
Bahasha
Vipeperushi
Tiketi za vyombo vya Usafiri
Mabango ya matangazo
kadi za Kila aina

Pia tunatoa huduma za:

Type Setting na Usanifu
Ukarabati vitabu Chakavu

Wasiliana nasi:

Moshi Lutheran Printing Press

S.L.P 301, Moshi

Kilimanjaro

Simu: +255 272 750 546

Mob: +255 752 327 899

Moshilutheranpress@gmail.com